# Bila Fedha Au Bila Gharama

Jeffersonville, Indiana, USA

Agosti 02, 1959

1 Hakika ni majaliwa kurudi hekaluni, asubuhi ya leo. Sijui tu … Ndugu Neville alisema ya kwamba wengi hawakuweza kusikia huko nyuma. Je, mnaweza kunisikia vizuri zaidi sasa, huko nyuma? Je! Ni sawa? Vema. Mimi ni—mimi ni mdogo, kwa hiyo inanibidi kupiga makelele sana ili watu wajue niko.

Kwa hiyo, ninakumbuka wakati mmoja nilipokuwa nikifanya kazi kwenye Huduma za Umma. Ninapanda kipandio … Nami nilikuwa nikivaa viatu vikubwa mno, vya njumu, kutokana na kutembea kwenye laini kubwa za umeme. Nami nilikuwa nikipanda vipandio. Na Bibi Ehalt, ambaye ni rafiki yangu, alikuwa kwenye ubao wa kubadilishia umeme. Nina hakika Bw.Ginther pale angemtambua, vizuri sana. Kwa hiyo Edith akasema, "Billy, unapiga makelele sana kuliko wote, kwa jamaa mdogo hivyo, niliyepata kumwona." Nikikanyaga kwa viatu hivi vya njumu, nikipanda vipandio.

Nikasema, "Vema, Edith, mimi ni mdogo sana, inanibidi kufanya kila mtu ajue niko huku, napiga kelele nyingi sana."

2 Vema, niliingia tu kupiga simu. Ndugu Neville alikuwa ameniambia ya kwamba rafiki yetu mzuri, Ndugu Roy Roberson, hayuko ibadani asubuhi ya leo, kwa sababu ya kuwa mgonjwa. Ninii yake … Alikuwa na jino lililopachikwa. Limesababisha maambukizi, na kumpa homa kidogo. Naye ataenda likang'olewe, nadhani, mara moja. Naye Roy amekuwa kama baba kwetu hapa, nasi tunampenda. Nami nikasema, "Ndugu Roy, ni—ninaingia sasa, katika dakika chache tu, kwenye ibada." Nikasema, "Nitaliuliza kanisa kwamba sote tutakuombea, asubuhi ya leo," na kesho atakapokuwa akienda huko, hili likashughulikiwe. Hilo jino limeota vibaya, ama kitu fulani, limeingia ndani vibaya, nao hawana budi kulikata, na kuling'oa.

3 Ndugu Roy ni mwanajeshi mstafu, kama mjuavyo nyote, kutoka kwenye Vita vya Pili vya Dunia, ambaye amepigwa risasi kweli kweli. Na kama isingalikuwa ni kwa ajili ya wema wa Mungu, hata asingeishi. Alilazwa nje miongoni mwa wafu, kwa muda mrefu; mikono imelipuliwa humu ndani, na miguu ikalipuliwa, na mishipa yote miwili mikubwa ikauawa. Naye daktari akasema, "Kama angaliishi, asingepiga hatua hata kidogo." Kwa neema ya Mungu, yeye hufanya kazi kila siku, akipanda na kila kitu. Mungu amekuwa mwema kwake kwa sababu yeye ni mtu mzuri, nasi tunampenda. Nasi, sisi—sisi sote si …

Kama tukiishi vizuri, hiyo haimaanishi ya kwamba hatuwezi kupata shida. Kwa kweli, inamaanisha ya kwamba shida zote zimeelekezwa kwetu. "Kwa maana mateso ya mwenye haki ni mengi, lakini Mungu humponya nayo yote." Hiyo ndiyo sehemu yenye utukufu.

4 Kwa hiyo tutaomba maombi maalum tu asubuhi ya leo, kwa ajili ya Ndugu Roy. Sijui kama kuna ye yote hapa ndani, bado, ambaye angetaka kuombewa, angetaka kukumbukwa katika neno la maombi? Kama wangeinua tu mikono yao. Vema. Hilo ni sawa. Hebu na tusimame kwa muda kidogo tu, mkiweza, tunapoomba.

5 Bwana, tunakuja leo, mwanzoni mwa sabato. Na jua linachukua mkondo wake sasa, kuruka kote ulimwenguni, kuleta nuru na uhai kwa mambo hayo ambayo limekusudiwa kufanya hivyo. Na mwanzoni mwa ibada ambayo … Sisi ni sehemu ya Kanisa Lako, ambalo limeitwa kushikilia ibada za uponyaji, uponyaji wa mwili kwa mwili; kutimiza matakwa na mapenzi ya Bwana wetu mbarikiwa Ambaye alijeruhiwa kwa makosa yetu, na kwa kupigwa Kwake sisi tuliponywa. Nasi tungeomba, mwanzoni mwa ibada, inapoanza kuchukua mbawa zake, katika nyimbo, na mioyo yetu inaanza kuinuliwa, kwamba tungekumbuka, asubuhi ya leo, Bwana, ndugu yetu mpendwa, mpendwa, Roy Roberson , Mtumishi Wako mnyenyekevu. Nasi tunajua ya kwamba Wewe uliyaokoa maisha yake kwenye uwanja wa vita, nawe umekuwa mwema kwake. Na leo hii anaugua kwa mateso, hata asingeweza kuhudhuria kanisa.

6 Na, Bwana, walipokuwa wakiomba katika nyumba ya Yohana Marko, kulikuwako na Malaika aliyeshuka akaingia gerezani, ambapo Petro alikuwa kifungoni, hapo alifungua milango, kisiri, na kumtoa nje.

Ee Bwana, Wewe ungali Mungu. Malaika hao wako chini ya amri Yako asubuhi ya leo. Tunaomba, Bwana, ya kwamba wakati tunapoomba hapa katika nyumba ya Mungu, ya kwamba Malaika watashuka kwenda nyumbani kwa Ndugu Roberson. Shauku yake ni kuwa mahali pake hapa, bali mateso yamemzuia. Na jalia Malaika wa Mungu wamwokoe, wamfanye mzima, ili aweze kuchukua mahali pake tena katika nyumba ya Mungu.

7 Kuna wengine ambao wamepitia magumu, wao—wao wamekuwa wagonjwa. Nasi tulimwona mwanamke mzee, alipokuwa karibu kuketi, akiinua mikono yake, alipokuwa akitembea dede kwa miguu yake. Amekuja katika nyumba ya Mungu, kuponywa. Jalia, Bwana, kwamba atatoka akitembea, akiwa na chemchemi na ujana wa msichana.

Wengine wote walioinua mikono yao, mingi iliinuliwa juu, maana imeandikwa, na imenukuliwa hapo awali, "Mateso ya mwenye haki ni mengi, lakini Mungu humponya nayo yote." Jalia leo turuke tuingie kwenye imani, mikono ya imani, ambayo itatuokoa na magonjwa na mateso yote. Wakati ibada itakapokwisha, jalia kusiwe na mtu mnyonge miongoni mwetu.

Jalia, Bwana, ya kwamba kila asiyeamini atakuwa mwamini. Na tunapotafakari juu ya Neno Lako, jalia Roho Mtakatifu alichukue na kuliweka mioyoni mwetu, na hapo alimwagilie maji mpaka lipate kuwa tunda la Neno. Fanya jambo hili kwa ajili yetu, Bwana, tunapoinamisha vichwa vyetu kwa unyenyekevu na kuomba katika Jina la Yesu. Amina.

Mnaweza kuketi.

8 Kabla tu ya kuingilia ujumbe wa ibada ya asubuhi ya leo, ningependa mweke akilini mwenu, kwa karibu zaidi. Iwapo kuna yeyote wenu aliye na likizo, na angependa kuhudhuria mojawapo ya ibada zitakazofanyiwa Middletown, Ohio, kuanzia Jumatatu, juma lijalo, itakuwa kwenye vile viwanja vya kambi.

Je! Unajua jina la hivyo viwanja vya kambi, Gene? [Ndugu Gene anasema, "Kasema ilikuwa maili kumi na mbili kutoka Middletown." — Mh.] Ndugu Sullivan. Middletown ni mji mdogo, nadhani kama Jeffersonville hapa. Ni kituo cha mpira wa vikapu. Ndugu Sullivan ndiye mchungaji pale. Yeyote wa makanisa ya Full Gospel, ambapo kuna sitini na kitu yanayoshirikiana katika mkutano huu, ataweza kuwaambia viwanja vya kambi vilipo.

9 Na kutakuwa na vibanda vingi kwenye viwanja hivyo, ninasikia, kuwashughulikia watu ambao wangependa kuja. Na mikutano itaanza Jumatatu hadi Jumamosi, siku sita. Na haitakuwa Jumapili, kwa sababu ya makanisa mengine, kwamba wanaweza kwenda kufanya ibada zao za kawaida. Labda, kutakuwa na ibada za uponyaji, ama maombi kwa ajili ya wagonjwa, kila usiku. Na kila mtu amealikwa. Nayo mikutano itaanza Agosti 10, hadi 15, Jumatatu hadi Jumamosi. Na kama una likizo, na—na likizo yako inakuja, na ungetaka kuitumia kwa njia hiyo, vema, hakika tungefurahi kuwa nawe.

10 Pia ningependa kuwahimiza wale wote ambao hawajabatizwa katika ubatizo wa Kikristo, kubaki asubuhi ya leo na kutafakari hilo. Nawe uwe tayari kwa ajili ya ibada ya ubatizo itakayofuata katika dakika kama arobaini na tano sasa, nadhani. Hilo litakuwa hapa kanisani.

Tunapenda sana kuwahimiza watu wabatizwe katika ubatizo wa Kikristo, tukijua ya kwamba ni muhimu kwa wokovu. Kwa maana iliandikwa na Bwana wetu, agizo Lake la mwisho, agizo Lake la mwisho kwa Kanisa. Ama, kama alivyoliamuru Kanisa, mwisho, Yeye alisema, "Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe. Yeye aaminiye na kubatizwa ataokoka." Kwa hiyo tunajua ya kwamba ni muhimu kwamba tubatizwe kwa kuzamishwa.

11 Na tutafurahi kukupa huduma hii, kwa mtu yeyote aliyeshawishika moyoni mwao ya kuwa Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu, ya kwamba alikufa ili awaokoe wenye dhambi, nawe ndiwe ambaye Yeye alikufa apate kuokoa; na ungependa kuja na kubatizwa katika Jina la Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi zako; ukiuambia, ulimwengu, ya kwamba unaamini kwamba dhambi zako zimeondolewa, na kwamba sasa utakuwa mfuasi wa Bwana Yesu, kuchukua msimamo wako.

12 Kama huna kanisa la kuhudhuria, tungefurahi ukishiriki pamoja nasi. Hatuna wafuasi hapa. Ni maskani iliyo wazi, kwa ajili ya Mwili wote wa Kristo, wa kila dhehebu. Tunasimama kama wasiojifunga na madhehebu. Nasi tunafungua milango kwa watu wote, haijalishi wao ni nani, rangi, jamii, au kanuni ya imani, kila mtu amekaribishwa. "Atakaye, na aje." Na kama huna kanisa lingine, tungefurahia wewe kuja tu na kushiriki pamoja nasi. Hakuna cha kujiunga nacho. Ingia tu moja kwa moja wakati milango imefunguliwa, na ushiriki pamoja nasi. Hilo tu ndilo unalohitaji; njoo tu namna hiyo. Njoo kwa moyo ulio wazi, ushikane nasi, na utusaidie tunaposonga mbele kwa ajili ya Ufalme-wa-Mungu. Kwa kuwa, tunaamini ya kwamba ile saa, itakapokaribia, ambapo mambo yote yaliyonenwa katika Biblia yatatimizwa.

13 Hapana shaka wengi wenu mlisoma ninii ya Khrushchev, taarifa yake kwa U.N., hivi majuzi, kama ilivyonukuliwa kwangu kutoka kwenye gazeti la Canada, na rafiki. Yeye alisema, "Kama kuna Mungu, Yeye yuko tayari kulifuta na kulisafisha hekalu tena, pamoja nanyi mabepari, kama alivyofanya hapo mwanzo." Kwa hiyo sasa unaweza kusoma katikati ya mistari, "Yeye yuko tayari kulifuta hekalu tena." Na ni mbaya sana, mkomunisti angepaswa kusema jambo kama hilo? Alikuwa na kitu fulani, hata hivyo. Hiyo ni kweli. Ilikuwa ni mabepari, hapo mwanzo, waliosababisha shida. Sisi ni mabepari.

14 Nilimsikia mchungaji wetu mpendwa, Ndugu Neville, akitoa tamshi kwenye televisheni yake … ama kipindi cha redio, hivi majuzi asubuhi, ambalo lilijirudia tu tena na tena, akilini mwangu. Siwezi tu kulisahau. Nilimnukulia rafiki yangu, jana usiku. Na hiyo ilikuwa hivi, kwamba kutakuwa na … Baada ya kuondolewa kwa Roho Mtakatifu, kutoka duniani, hiyo dini rasmi ya kanisa itaendelea moja kwa moja, bila kujua tofauti yake. Je, umewahi, ulininii… Ni wangapi waliosikia hayo? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Hilo halikuwa ni la kushangaza? Wao hawamjui Roho Mtakatifu, kwa hiyo hawatajua wakati Yeye ameondoka, nao watakuwa wakiendelea tu vivyo hivyo. Wakati yule wa mwisho ametiwa muhuri katika Mwili wa Kristo, watakuwa wangali wanaendelea, wakijaribu kuwaleta waongofu Kwake, kwa maana hawajui kile alicho. Na dini zao za kawaida zitaendelea tu kama walivyokuwa. Sasa, huenda lisiingie ndani yako kama lilivyonipata mimi, bali hilo kwa kweli lilikuwa ni tamshi la kushangaza. Kwamba, watakuwa mbali sana, katika taratibu za kidini, mpaka hawatamkosa Roho Mtakatifu, kwa sababu hawajui ni kitu gani, kwanza.

15 Mungu aturehemu. Ndugu, ningependa kuishi katika maisha haya, na shauku yangu, mpaka kama hata ni ile huzuni Yake iliyo ndogo sana, nitaijua moyoni mwangu. Nikifanya jambo ambalo lingemhuzunisha Yeye, ningeweza kuihisi katika muda mfupi tu.

Achilia mbali, kutokuwepo Kwake; Sitaki kuwa hapa wakati Yeye hayupo hapa. Ninataka kuondoka basi, naam, bwana, kwa kuwa hakutakuwa na Damu kwenye kiti cha rehema. Kutakuwa na giza na moshi na kweusi. Madhabahu haitakuwa na Wakili pale, kuitetea kesi yetu wakati huo. Mnajua Maandiko yanasema hivyo? Madhabahu yalikuwa yakitoka moshi. Hapakuwapo na Damu kwenye kiti cha rehema, basi ni hukumu.

Kama Bwana, mapema msimu huu wa majani kupukutika, atatupatia uamsho wa siku chache usiku. Nimeliweka tu niani mwangu, ninataka kukichukua Kitabu cha Ufunuo, kwa kukisoma, tupitie tu moja kwa moja katika Kitabu cha Ufunuo, na kuendelea.

16 Sasa, leo, ninajua ya kwamba kuna wengi wanaoingia, kuombewa. Na ofisi yangu ilifungwa leo, ama juma hili. Na baadhi ya watu walikuwa wamekuja, hawakupata nafasi ya kuombewa, huko nje, kwa sababu hao wavulana walikuwa wameondoka, kwa siku moja au zaidi, wapate kupumzika. Wana kazi nyingi za kufanya; kazi zao wenyewe, pamoja na kazi ya maskani, na simu zangu na kila kitu. Baadaye kidogo linakutia wasiwasi. Na kwa hiyo basi hiyo ndiyo sababu. Ninajua sina budi kutoka mahali fulani, mara kwa mara, na kufanya jambo fulani tofauti, nami ninajua wanafanya hivyo, pia. Kwa hiyo, wakaniita. Nikasema, "Nafikiri ingekuwa sawa." Nasi tutawaombea wagonjwa, katika dakika chache.

17 Nami nilifikiri tungesoma baadhi yake kutoka kwenye Neno la Mungu. Kama una Biblia yako sasa, hebu na tufungue Kitabu cha Isaya. Ninapenda kukuona ukichukua Kitabu chako na kukisoma. Ninasoma … Kama si zaidi ya Neno moja ama mawili tunayosoma, hata hivyo, Ni Neno la Mungu la Milele, Lisilokufa. Haliwezi kupita kamwe. Mlango wa 55 wa Isaya, mada, "Wokovu wa milele."

> *Haya, kila aonaye kiu, njoni majini, na yeye asiye na fedha; njoni, nunueni, mle; naam, njoo, ununue divai…maziwa bila pesa na bila gharama.*
>
> *Kwa nini mnatoa pesa kwa kitu ambacho si mkate? na kazi yenu kwa yale yasiyoshibisha? nisikilizeni kwa bidii, mle kilicho chema, na nafsi zenu zifurahie unono.*
>
> *Tegeni masikio yenu, mkanijie: sikieni, na nafsi zenu zitaishi; nami nitafanya nanyi agano la milele, rehema za hakika za Daudi.*

Ningetaka kuzungumza nanyi, kwa muda mfupi tu, juu ya somo: Bila Fedha Au Bila Gharama.

18 Kuna mambo mengi sana ya kufurahisha katika siku zetu. Kuna mengi sana ya kuwashawishi watu kwenye yale tungeyaita "anasa," na ni kwa ajili ya watu wote, nyakati zote.

Kuna vishawishi vya vijana, ngoma za kisasa na karamu za roki, na muziki walio nao unaoambatana nayo. Na yote yanavutia, kwa ajili ya burudani.

Sijali mtoto amelelewa katika nyumba nzuri iliyoje, na jinsi amefunzwa kutenda mema; ikiwa mtoto huyo hajakubali ujuzi wa Kuzaliwa upya, muziki wa roki huvutia usikivu wake haraka mara tu anapousikia. Kwa sababu, ndani yake, kwa maumbile, imezaliwa ndani yake, roho ya kimwili. Na nguvu za Ibilisi ni kuu sana, leo, mpaka zinashika roho hiyo ya huyo mtoto.

19 Na ni zaidi sana iliyoje zitawafanyia wazee, basi, ambao wamekataa Kuzaliwa upya! Kwa sababu, ni wakati tu maisha yako yamebadilishwa, nawe umeongoka na kuzaliwa upya, katika Ufalme wa Mungu, asili yako bado itakuwa ya mambo ya ulimwengu, haijalishi wewe ni wa kidini jinsi gani, isipokuwa hiyo imebadilishwa ndani yako. Ungeweza kuabudu na kuwa wa kidini, lakini bado hiyo itakuwa na aina fulani ya nguvu za kukuvutia, kwa sababu mtu huyu wa kale wa dhambi na tamaa zake hajafa ndani yako bado.

Lakini mara tu Kristo anapotawazwa moyoni mwako, mambo hayo hayasumbui. Ni kitu kikuu zaidi.

20 Siwezi kulitaja jina la mtu huyo, maana siwezi kukumbuka jina lake sasa, bali wengi wenu mtamkumbuka. Wanasema kulikuwa na kisiwa ambamo wanaume wangeenda, kwa kuvizia, na wanawake wangetoka, wakiimba. Nazo nyimbo zao zilikuwa za kutamanisha sana, hata mabaharia waliokuwa wakipita, kwa meli, wangeingia. Ndipo askari wa kuvizia wange—wangewakamata mabaharia hawa wasiojihami, na kuwaua. Basi mtu mmoja mkubwa alitaka kupitia pale. Naye akawaamuru mabaharia wake wamfungie kwenye nguzo ya mlingoti, na—na—na kuweka kitu kinywani mwake, ili asiweze kupiga kelele; kisha—kisha akaweka vizibo masikioni mwa mabaharia wake, wasiweze kusikia, ndipo wapitie pale, kusikia. Basi wale wanawake wakatoka, wakicheza na—na kupiga makelele, na kuimba, na, loo, zilikuwa nzuri sana, hata akaing'oa ngozi kwenye vifundo vya mikono yake, akiwapigia makelele mabaharia wake, "Geukeni mwingie! Geukeni mwingie!" Lakini hawakuweza kumsikia, walikuwa na vizibo masikioni mwao.

21 Ndipo basi akapita baharini mpaka mahali fulani ambapo wangemfunua, au, kuifungua mikono yake,

naye alipaswa kutoa vile vizibo masikioni mwao. Huko, wakati akitembea mitaani, alisikia mwanamuziki ambaye alikuwa bora zaidi kuliko hao huko chini, hata alipopita pale tena, walisema, "Loo, ewe haramia mkuu wa baharini, tukufunge kwenye nguzo ya mlingoti tena?"

Akasema, "La, niache huru tu. Nimesikia jambo kubwa zaidi, hata hilo halitanisumbua tena."

Hivyo ndivyo ilivyo kwa Mkristo aliyezaliwa mara ya pili. Walipata kitu fulani kikuu zaidi kuliko roki na burudani za ulimwengu huu. Wanaburudishwa na Roho Mtakatifu. Ni bora zaidi, hata ulimwengu umekufa kwao.

22 Lakini unapoenda kwenye burudani hizi rahisi, lazima ukumbuke ya kwamba huna budi kuchukua pesa nyingi sana. Jamaa mdogo anayemchukua rafiki yake wa kike kwenye karamu hizi na dansi hizi, na kadhalika, atalipa sana mapato yake ya juma. Nao wazee ambao wanajaribu kupata raha katika kwenda kwenye vyumba vya pombe, kuzinywea huzuni zao za juma, itawabidi kulipa pesa nyingi. Na wanapata nini kutokana nayo? Hawapati kitu ila maumivu ya moyo.

23 Na kumbuka, huna budi kukaa na Mungu siku moja kwa jambo hilo. "Na mshahara wa dhambi ni mauti." Hufanyi kitu hapa duniani, kwa jambo hilo. Ni mazigazi ya uongo. Kunywa pombe kutaongeza tu huzuni. Dhambi itaongeza tu mauti juu ya mauti. Cheki yako ya mwisho itakuwa ni kutengwa na Mungu, Milele; utupwe katika Ziwa la Moto. Wala huwezi kupata kitu cho chote, ila kupoteza.

Ndipo Mungu anakuja na kuuliza swali, "Kwa nini mnatumia fedha zenu kwa ajili ya mambo yasiyoridhisha? Kwa nini mnafanya jambo hilo?"

Ni kitu gani kinachomfanya mwanadamu atake kufanya jambo hilo? Wanatumia yote waliyo nayo, yote wanayoweza kupata, kununua pombe, kuwavisha nguo wanawake wanaozurura nao, ama namna fulani ya anasa chafu, za ulimwengu.

Lakini tunaambiwa katika Biblia, na tunaalikwa kumjia Mungu, "Na kununua furaha ya Milele na Uzima wa Milele, bila fedha wala gharama."

24 Mambo hayo hayawezi kuridhisha, na mwisho wake ni mauti ya Milele. Na inakugharimu pesa zote unazoweza kukusanya pamoja, kuwa m—mtu mkubwa au mburudishaji, ama mvulana mcheshi, ama chochote unachoweza kuwa, ama msichana maarufu, ama chochote kile. Inagharimu yote unayoweza kukusanya pamoja, kufanya hivyo. Kuvaa mavazi nadhifu mno, na—na kufanya mambo ambayo ulimwengu hufanya, ndipo unaishia tu kupata cheki ya laana ya Milele.

25 Mungu alisema, basi, "Kwa nini?" Tutafanya nini kwenye Siku ya Hukumu, tutakapoulizwa ni kwa nini tulifanya hivyo? Jibu letu litakuwa nini? Itakuwaje jibu kwa Marekani ya kisasa, ambao husema ya kwamba wao ni taifa la Kikristo? Na kuna pesa nyingi zinazotumiwa kwa wiski, katika mwaka mmoja, kuliko zilizopo kwa ajili ya chakula. "Kwa nini utumie pesa zako kwa mambo kama hayo?" Hata hivyo, serikali ingekufunga gerezani, kwa kodi ya dola tano ulizokuwa umetuma labda kwa taasisi fulani ambayo haikuwekwa ipasavyo ipate kupokea kodi, kupeleka baadhi ya wamishenari katika nchi za ng'ambo. Tutaulizwa siku moja, "Kwa nini mlifanya hivyo?"

26 Sisi ni taifa la Kikristo, na mabilioni yanatumiwa watu hao huko, ambao tunajaribu kununua urafiki wao. Sasa wanaukataa. Si ajabu Khrushchev alisema, "Ikiwa kuna Mungu, atalifagia jumba Lake la kifalme tena." Makafiri wanaweza kutoa matamshi kama hayo, wapate kutuaibisha. Ni kitu cha dhihaka iliyoje! Nasi tunajiita Wakristo.

Mungu alisema, "Njoni, mnunue Uzima wa Milele, bila fedha, bila gharama." Uzima, kuishi milele, nasi tunaupa kisogo na kucheka usoni Mwake. Tutafanya nini Siku hiyo? Itakuwaje …?

Ikiwa Mungu anatupa vitu vya kufanya, na kutupa pesa, na kutufanya kuwa taifa tajiri kuliko yote chini ya mbingu, basi Mungu atauliza, tulifanya nini nazo. Kwa nini tunatumia fedha zetu kwa mambo yasiyoridhisha? Sio tu kwa taifa, bali hiyo itakuwa kwa watu binafsi; kuanzia mapeni, hadi mamilioni ya dola, kila mmoja atapewa.

27 Wakati watu wanapouana: nilisoma makala hivi majuzi tu, ambapo wavulana wawili waliofanya kazi katika kambi moja ya uwindaji. Mmoja alikuwa na watoto watano, mwingine alikuwa na wawili. Na mmoja wao ilibidi aachishwe kazi. Basi mmoja wa hao wavulana aliyekuwa na watoto wawili, au aliyekuwa na watoto watano, akajisikia kwamba alihitaji hiyo kazi zaidi ya yule aliye na watoto wawili; basi akaenda kuwinda pamoja naye, na kumpiga risasi mgongoni.

Pesa, ni taifa la namna hiyo, ni hisia ya namna hiyo, hiyo ndiyo aina ya roho inayowatawala watu.

Ndipo unaweza kuona jinsi ambavyo Kuzaliwa upya kunapaswa kuwa muhimu. "Huna budi kuzaliwa mara ya pili." Haina budi kuwa. "Njoni Kwangu, mkanunue bila fedha."

Huwezi kusema, "Sikuwa na pesa." Huhitaji pesa zozote. Inatolewa bure.

28 Sisi Wamarekani tumezoea kulipia kila kitu. Huo ndio kauli mbiu yetu. "Tunalipia vitu. Tuna fedha." Tunapeperusha noti zetu za dola kwa nchi zingine, na kadhalika, zilizo maskini. Wanaingia, unaona watalii wakiingia, wote wako katika hali nzuri na wazima. Wamarekani huyashughulikia hayo. Mambo hayo ni mapato ya aibu mbele za Mungu. Hayo hayatailipia safari yetu ya kwenda Mbinguni. Lakini kila kitu Marekani, inatubidi kuilipia safari yetu.

Unaingia mkahawani, nawe unakula chakula chako cha kutwa. Na ikiwa hutaweka pesa mezani, kumpa bakshishi mhudumu huyo, atakunja uso, huku analipwa na kampuni anayoifanyia kazi. Na hiyo ingefaa iwe angalau asilimia kumi, au zaidi, ya bili yako. Usipofanya hivyo, mhudumu huyo atakudharau kama mchoyo au aina fulani ya—ya bahili. Wakati, yeye analipwa pesa zake. Nafikiri ni fedheha na aibu, kufanya hivyo. Nafikiri ni uamuzi mbaya kwa taifa. Zamani, watu wazuri, mahali pazuri, hawangeruhusu hilo. Lakini yote yanaingia katika roho moja kubwa.

29 Nilikuwa nikisafiri, kwenye gari moshi. Na bawabu … Nilikuwa nimeshika mkoba mdogo kwa mkono mmoja, sanduku la nguo kwenye mkono mwingine, na kijisanduku changu kidogo cha kunyolea chini ya mkono wangu, nami nilikuwa nikitembea. Huyo bawabu akanijia, akasema, "Je, ninaweza kukubebea?"

Nikasema, "Loo, ninaenda tu moja kwa moja kwenye gari moshi, bwana. Asanteni, sana." Karibu tu, loo, yadi thelathini.

Akasema, "Nitakibeba," ndipo akachukua hicho kitu kidogo na kukibeba, akatembea.

Vema, alipofika, nilifikiri labda mimi… Nilijua alilipwa, lakini ningempa tu—ningempa tu nusu dola. Pengine alikuwa anao, mzigo wangu, kwa yapata, tuseme, dakika moja; yapata urefu wa maskani hii, ambapo alifikia kwenye gari-moshi. Nikaingia kwenye gari-moshi, kwanza, ndipo nikaunyosha mkono na kulichukua. Nilimpa nusu dola.

Akasema, "Hebu kidogo!"

Nikasema, "Kuna nini, bwana?"

Akasema, "Nilikubebea mifuko mitatu!"

Nikasema, "Naam, bwana, hiyo ni kweli. Nini, nini mbaya?"

Akasema, "Malipo yangu ya chini kabisa ni senti ishirini na tano kwa mfuko. Ninakuwia senti zingine ishirini na tano."

Mnaona, huo ni Umarekani, kila kitu hakina budi kulipiwa.

30 Ukienda kuliendesha gari lako nalo lianguke katika handaki, nawe umwite mtu fulani kukuvuta utoke. Afadhali uwe tayari kulipa, maana watakulipisha kwa hiyo. Mvutaji akija na kukutoa, atakutoza kiasi fulani kwa maili. Na endapo mkulima, mara tisa kutoka kwa kumi, akileta trekta yake, itakuwa ni mbaya kuliko hivyo.

Huna budi kulipia kila kitu unachofanyiwa. Kila kitu ni "Lipa! Pesa! Lipa! Pesa!"

Na hata hivyo ni shimo kubwa jinsi gani dhambi imekutumbukiza! Ni nani angaliweza kukutoa kwenye shimo la dhambi? Lakini Mungu anakutoa kwenye shimo la dhambi, bila pesa, bila gharama, wakati hakuna mtu anayeweza kukutoa.

Usipolipa pesa nyingi za kuvutwa na mvutaji wako, utakaa katika hilo shimo. Huna budi kuwa na pesa la sivyo utabaki shimoni.

31 Lakini shimo baya zaidi ulilopata kuingia, ni lile ibilisi alilokutupa ndani, shimo la dhambi na kutokuamini. Mungu kwa kupenda kwake atakutoa huko, bila pesa, bila gharama. Na hata hivyo unakaa shimoni, ukigaragara tu dhambini, wala hata humwiti Yeye.

Unapomleta mwenye kuvuta, kwa kawaida huweka mnyororo mkubwa humo ndani kabisa ya shimo, anaufunga kwenye bamba au popote pale, kisha anaanza kuuzungusha mpini. Ndipo nguvu za hilo gari zinaanza kuvuta, nayo mota inaanza kufanya kazi, na kukutoa.

32 Mungu anapokupata kwenye shimo la dhambi, na kukusikia ukimwita, Yeye hushusha mnyororo uliokuwa umefungiwa Kalvari, upendo wa Mungu, na kuushikiza moyoni mwako, na kuweka Nguvu za Roho Mtakatifu mle, zianze kuvuta. Wala haikugharimu kitu. Na hata hivyo tunalala shimoni kwa sababu hatuwezi kulipa kwa mifuko yetu. Sisi Wamarekani tunafikiri tunaweza kulipa kutoka mifukoni mwetu, bali huwezi. Ni bila pesa au bila gharama. Hulipii kanisani. Yesu aliilipa pale Kalvari. Lakini watu wanalionea haya. Wanalitaka kwa njia yao. Mungu anayo njia kwa ajili yako kuipokea, na ni bure kama utaipokea.

33 Kwa kawaida, wanapokutoa shimoni, umekwaruzwa kabisa, huna budi kwenda, hospitalini. Na kabla hawajaanza kukufanyia kazi, kabla jambo moja halijatendeka, wanauliza, "Ni nani atakayelipa hiyo bili?

Ikiwa tutavishona hivi vidonda, ikiwa tutavimiminia mafuta, na kukudunga sindano za—za kukuchanja kukukinga na sumu ya damu, una bima ya aina gani?" Kabla hawajafanya jambo moja, lazima iwe ni pesa kwanza.

34 Lakini wakati Bwana wetu anapouweka mnyororo Wake wa upendo kuzunguka moyo wako, na kukuvuta kutoka kwenye shimo la dhambi, Yeye huponya kila moyo uliovunjika, anaondoa dhambi zote. Na hiyo bili imewekwa katika bahari ya usahaulifu, isikumbukwe dhidi yako tena. "Njoo, bila pesa au bila gharama." Haidhuru umekatakatwa vibaya jinsi gani, umejeruhiwa vibaya jinsi gani, jinsi familia yako imefanya, wala yale umefanya, hakuna deni kwake. Yeye huponya maumivu ya moyo, anakuondolea huzuni zako zote. "Alijeruhiwa kwa makosa yetu, akachubuliwa kwa uovu wetu; adhabu ya amani yetu ilikuwa juu Yake; na kwa kupigwa Kwake sisi tuliponywa." Yote ni bure.

Nasi hatutampokea, ni kwa sababu tumetawaliwa na roho mbaya. Tunatawaliwa na roho ya taifa, roho ya ulimwengu, badala ya kutawaliwa na Roho wa Mungu, Roho Mtakatifu, ambaye hutuongoza na kutuelekeza kwenye Kweli zote, na kuitimiza Biblia.

35 Wakati fulani uliopita, nilikuwa nikizungumza na kafiri. Akasema, "Wazia jambo hilo, Bw. Branham. Taabu hii yote ya maisha, na kitu pekee tulicho nacho, kwamba tumeokoka, ni maandishi fulani ya kale ya Kiyahudi."

"Loo," nikasema, "bwana, hayo yanaweza kuwa ndiyo yote uliyo nayo, lakini mimi nina kitu zaidi ya hayo. Ninaye Roho wa Yule aliyeyaandika, anayeyathibitisha na kuyatimiza, kila ahadi." Hakujua jinsi ya kulichukua hilo.

Mnaona, huna budi kuja na kununua bila fedha, kununua bila gharama. Haigharimu chochote. Ni bure kwa "atakaye, na aje." Mungu anakuvuta kukutoa shimoni.

36 Kama vile yule mtu kwenye lango liitwalo Zuri. Alikuwa ametupwa shimoni, kutoka tumboni mwa mama yake, na ibilisi ambaye alikuwa amemlemaza miguuni. Njia yake ya kujipatia riziki ilikuwa ni kuomba msaada kutoka kwa watu waliopitia hapo. Na alipoketi langoni asubuhi hiyo, aliwaona wahubiri wawili wa kipentekoste wakija. Hawana hata senti moja miongoni mwao, kwa maana alisema, "Sina fedha." Na senti ndiyo kipande kidogo zaidi cha fedha. "Sina fedha wala dhahabu."

Nadhani mtu huyo aliwazia kitu kama hiki. "Hakuna haja ya kuchukua kikombe changu." Labda alikuwa akijaribu kuweka akiba pesa ya kutosha. Alikuwa na umri wa miaka arobaini, na labda alikuwa akijaribu kuweka akiba ya pesa za kutosha, madaktari wangeweza kumtengenezea jozi ya magongo, ya kutembelea, kwa kuwa, yeye, alidhoofikia kwenye vifundo vyake. Na labda ilimbidi awe na pesa, kusimama mstarini, kabla madaktari hawajamsaidia. Na kwa kweli hakuna haja ya yeye kuwainulia kikombe chake wahubiri hawa wa kipentekoste ambao hawakuwa na kitu. Fursa, wao…alikuwa maskini sana, kuwahi kupata senti moja kutoka kwa watu hao.

37 Lakini wakati alipoangalia usoni mwao! Mmoja, mchanga na mwenye soni kwa ujana; huyo mwingine, mzee na ana mikunjo; kama Yohana…Petro na Yohana walipofika langoni. Aliona kitu fulani katika kijana huyo. Hiyo ni, haya yake kidogo ilizidi ya kawaida. Aliona chini ya makunyanzi na taabu, za jua la Galilaya lililokuwa limeuchoma uso wa huyo mzee mvuvi, kulikuwa na "furaha isiyosemeka, na iliyojaa utukufu." Aliona kitu ambacho kilionekana kuwa tofauti kidogo.

Mnajua, kuna kitu kuhusu Ukristo, kinachowafanya watu waonekane tofauti. Ndio watu wenye kuvutia sana kote ulimwenguni.

Basi akachukua kikombe chake na kukiinua.

38 Naye mtume Petro, akiwa ndiye mkubwa kuliko wote, alisema, "Sina fedha wala dhahabu." Kwa maneno mengine, "Siwezi kukusaidia kwa vyovyote, kununua magongo haya. Sina fedha wala dhahabu, lakini nilicho nacho!" Alikuwa ametoka kununua kutoka Kwake aliyekuwa na asali na furaha ya divai ya wokovu. Alikuwa ndio kwanza aje, siku mbili ama tatu kabla ya hapo, kutoka Pentekoste, ambapo jambo fulani lilikuwa limetukia.

Ndipo huyo kijana akaruka na "amina" kubwa kwake, na kumtazama usoni mwake.

Kulifanyika nini? Msururu huo wa huruma, huruma yake Yeye aliyesema, "Niliwahurumia wagonjwa," Roho yule yule alikuwa amechukua mahali moyoni mwa yule mzee mvuvi. Alisema, "Kuhusu pesa, sina yoyote, lakini nina kitu ambacho kitachukua mahali pake mara milioni moja. Nilicho nacho!"

39 Sasa kumbukeni, Petro alikuwa Myahudi, nao wanapenda pesa, kwa kawaida, lakini Myahudi huyu alikuwa ameongoka. Sio, "Nilicho nacho, nakuuzia."

Lakini, "Nilicho nacho, ndicho nakupa! Nilicho nacho! Sina hata senti mfukoni mwangu. Nisingeweza kununua mkate mmoja. Nisingeweza kununua chochote. Sina hata senti. Lakini kama unaweza kuipokea, nilicho nacho, nitakupa kwa sababu nilipewa." Hicho ndicho tunachohitaji. "Nilicho nacho, ndicho nakupa."

"Una nini, bwana?"

"Nimekuwa Kwake anayeuza maziwa na asali, bila gharama. Nitakupa. Sikuwii chochote kwa ajili Yake. Kama unaweza kukipokea, nitakupa. Sio kama mtu ambaye angetoza, bali wale ambao wangetoa."

40 Kwa sababu, "Kadiri unavyopokea bure, toa bure." Ilikuwa ni agizo la Bwana wake, siku tatu tu kabla. "Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili. Yeye aaminiye na kubatizwa ataokoka; na asiyeamini atahukumiwa. Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio: Katika Jina Langu watatoa pepo; watanena kwa lugha mpya; wakinywa vitu vya kufisha, havitawadhuru; wakishika nyoka, haitawasumbua. Kadiri mlivyopata bure, toeni bure." Huyo Myahudi alikuwa amebadilishwa. [Ndugu Branham anagonga mimbara mara nne — Mh.]

Tunachohitaji Marekani ni kubadilishwa, kwa Roho Mtakatifu kuchukua mahali pa baadhi ya taratibu zetu za kidini. "Kwa kadiri mnavyopokea bure, toeni bure."

"Nilicho nacho, nakupa: Katika Jina la Yesu Kristo wa Nazareti, simama utembee"; imani katika hilo Jina lisiloghoshiwa la Muumba! Si ajabu alienda akirukaruka kwa furaha, na kumsifu Mungu!

41 Loo, mnajua mambo makuu, labda alikuwa ameketi pale miaka arobaini, akijaribu kupata fedha za kutosha kumnunulia magongo, bali asingeweza kufanya hivyo. Lakini katika mahali pasipotarajiwa kabisa, na wakati usiotarajiwa, na watu wasiotarajiwa kabisa, wasiostahili, alipata alichotaka. Nina furaha sana kwamba Mungu hufanya hivyo.

Katika kundi la maskini, wanaowaita watakatifu wanaojiviringisha usiku mmoja, nilipata nilichotaka, ambacho pesa haingeweza kununua. Katika kundi la watu wasiosoma, wasio na elimu, waliovalia vibaya, Wanegro, kwanza kabisa, huko nje katika maskini baa ndogo iliyogeuzwa, sakafuni, nilipata thamani, kito; wakati maskini yule mtu mweusi aliponiangalia usoni, na kusema, "Je, umepokea Roho Mtakatifu tangu ulipoamini?" Loo, lilikuwa ni jambo nililotaka. Sikutarajia kulipata miongoni mwa watu hao, lakini walikuwa na kile nilichohitaji.

42 Umoja wa Mataifa siku hizi, hawangekubali tulicho nacho, lakini hicho ndicho wanachohitaji. Khrushchev, hao wengine wote, wanamhitaji Kristo, katika ubatizo wa Roho Mtakatifu. Itabadilisha mielekeo yao. Itawafanya wanaume, wanaowachukia, wawe ndugu. Itaondoa uchoyo, na kijicho na ugomvi; na kuweka upendo na furaha, na amani, wema na rehema.

Naam, katika mahali pasipotarajiwa, wakati mwingine ndipo unapata kile unachotafuta.

43 Wana wa Israeli wangetoa nini (nyara zote za Misri) wakati midomo yao ilipokuwa ikitoka damu, wakati ndimi zao zilipokuwa zikinig'inia kutoka kinywani mwao? Wangetoa dhahabu yote waliyowapora Wamisri, kwa ajili ya kinywaji kimoja kizuri cha maji baridi. Viongozi wao wa nyikani walikuwa wamewaongoza kutoka mahali pa rutuba na maji jangwani hadi mahali pa rutuba na maji jangwani, kutoka kwenye mitaro hadi kwenye chemchemi, lakini zote zilikuwa zimekauka.

Kisha kukaja, bila pesa au bila gharama! ikanena na nabii na kusema, "Unenee mwamba," kitu kilicho kikavu kuliko vyote nyikani, kitu kilicho mbali zaidi na maji. Hapo kiu yao ilikatwa, bila pesa au bila gharama. "Unenee mwamba." Si ulipe mwamba, bali "unenee mwamba."

44 Yeye angali ni Mwamba usiku wa leo. Yeye ni Mwamba katika nchi ya uchovu. Kama unasafiri katika nchi hiyo ya uchovu, unenee Mwamba. Si lazima umlipe; nena Naye. Naye ni msaada uliopo kabisa katika wakati wa mateso. Kama wewe ni mgonjwa, unenee Mwamba. Kama wewe ni mgonjwa wa dhambi, unenee Mwamba. Kama umechoka, unenee Mwamba.

Mnaona, ilionekana kana kwamba ingekuwa mahali popote… Ilionekana hivyo, kama hakuna maji huko chini katika sehemu ndogo ambako kulikuwa na chemchemi, kusingekuwako na maji juu ya mlima huo, kando ya mwamba. Mungu hufanya mambo kinyume na vile mwanadamu anavyofikiri. Mwamba, mahali pakavu sana jangwani, bali Yeye alisema, "Unenee Mwamba."

45 Leo hii, watu wamedanganywa sana. Wanafikiri kama wanaweza kwenda na kuyakariri maombi yao, wamlipe kasisi fulani awaombee dua chache, wailipie safari yao. Kama watajenga kanisa kubwa mahali fulani, na tajiri fulani atalifadhili, waendelee kuishi katika tamaa mbaya, awe na mtu mwingine wa kumwombea, anawazia hiyo imetosha. Mungu hataki pesa zako chafu. [Ndugu Branham anagonga mimbara mara tatu — Mh.] Chote atakacho ni kujitolea kwako na maisha yako yaseme Naye. Mungu amekupa pesa, usizitumie kwa mambo yasiyoridhisha. Zitumie kwa mambo yanayoridhisha. Lakini ili kuleta utoshelevu wa kweli, huwezi kuipata mpaka uzungumze na Mwamba.

Alitoa maji ya uzima, bila pesa au bila gharama. Wakanywa, na ngamia zao wakanywa, na watoto wao wakanywa, na ingali ni chemchemi inayobubujikia nyikani.

Na vivyo hivyo Yeye ndiye Mwamba siku hizi, katika nchi hii ya uchovu, kwa watu wanaoangamia. "Kila amwaminiye hatapotea, bali awe na Uzima wa Milele."

46 Angalia. Kila usiku, haikuwabidi kujisumbua kuhusu mkate. Mkate wao ulileltwa kwao, kila usiku, upya.

Tunaenda siku hizi kupata mkate. Endapo wewe ni ombaomba, nawe uende hapa dukani, na kusema, "Ningetaka mkate."

Angesema, "Nionyeshe, kwanza, robo yako. Sina budi kuwa na senti ishirini na tano kwa mkate huu."

Nawe una nini ukiupata? Hili ni jambo la kando kidogo, lakini umepata cha chini zaidi ambacho ngano inaweza kutoa. Wanatoa vi—vitamini zote kutoka kwake, pumba yote, na kuwapa nguruwe. Wanachanganya lundo la gundi ambalo hushikilia pumba pamoja, na kuipepeta, na kukanda mkate, uliotengenezwa kwa mikono michafu, yenye kinyaa, mara nyingi. Mnaona kile unachopata kwenye mkate wako, wakati mwingine, vipande vya nywele, na vitu vya unajisi, na vipande vya panya, na kila kitu kingine kinachoangukia mle kwenye tanuri hizo za mikate. Watu wenye dhambi wenye magonjwa ya zinaa, na kila kitu, wakiikanda. Kama ungeiona ikikandwa, hata hungeila. Na, hata hivyo, unalipa senti zako ishirini na tano la sivyo huupati.

47 Naye Mungu aliwalisha kila usiku, mkate uliotengenezwa kwa mikono ya Malaika; bila pesa, bila gharama. Na, siku hizi, mkate huo ulimwakilisha Kristo, Maisha ya kiroho, aliyeshuka kutoka Mbinguni, kuutoa Uhai Wake.

Naye Mungu huwapa watoto Wake, kila siku, ujuzi mpya. Mnakumbuka, kama waliuweka huo mkate hadi kesho yake, uliharibika.

Unamsikia mtu akizungumza kuhusu, "Naam, nimepata… Nitakuambia. Mimi ni Mlutheri. Mimi ni Mpresbiteri, Mbatisti. Mimi ni Mpentekoste," huo ni maskini mkate wa zamani uliotengenezwa kwa mikono. Hakuna lingine, mchafu tu, na umetengenezwa kwa mikono ya wanadamu.

Lakini unaposikia ujuzi wa ushuhuda, mpya, "Asubuhi ya leo, katika maombi, Roho Mtakatifu aliibatiza nafsi yangu upya," loo, ndugu, hicho ni Chakula cha Malaika. Anawalisha upya, kila siku, kutoka Mbinguni.

> Manyunyu ya baraka tunahitaji.
> Matone ya huruma yanatuzunguka,
> Lakini tunaomba tupate hayo manyunyu.

Loo, naam, mshushe kutoka Mbinguni, upya, Bwana, Kristo Mkate wa Uzima. Mtupe moyoni mwangu, na kunijalia niufurahie Uwepo Wake mkuu.

48 Hakika, walikuwa na shukrani. Walikuwa na shukrani. Naye mwanamume yeyote ama mwanamke aliyezaliwa kwa Roho wa Mungu, na kumpokea Roho Mtakatifu, daima atakuwa mwenye shukrani. Haijalishi ni nini kinachofanyika, utakuwa na shukrani.

Kama vile maskini mvulana mdogo, kipofu kule milimani, Benny mdogo, alizaliwa. Akiwa na umri wa kama miezi minane, mtoto wa jicho anaanza kukua machoni pake. Wazazi wake walikuwa maskini. Waliishi kwenye kilima kidogo cha udongo wa mfinyanzi. Nao walijua kwamba upasuaji huo ungeweza kuyaokoa macho ya mtoto Benny, apate kuona. Alikuwa mvulana sasa wa yapata umri wa miaka kumi na miwili. Wazazi wake wangeweza tu kupata ya kutosha kununua mkate na nyama kwa ajili ya mwaka mzima. Hawangeweza kumudu upasuaji huo.

49 Majirani wote, pamoja, walimwona mtoto Benny akijaribu kucheza na watoto wadogo huko nje, kipofu. Asingeweza kuona alichokuwa akifanya. Wakawa na huruma. Na kila mmoja, mwaka huo, alichangia sehemu ya ziada ya mazao. Walifanya kazi kwa bidii zaidi kidogo kwenye jua kali. Ndipo wakati mazao yalipouzwa katika msimu wa majani kupukutika, walichukua hizo pesa wakampandisha mtoto Benny gari moshi, wakamtuma kwa daktari.

Walifanikiwa kufanya upasuaji huo. Ndipo aliporudi, majirani wote walikusanyika wakati mtoto Benny aliposhuka kwenye gari-moshi. Macho yake madogo, maangavu yaking'aa. Akaanza kupiga mayowe na kulia, alipozitazama nyuso zao.

Mmoja wa makondakta akasema, "Mwanangu, upasuaji huo ulikugharimu nini?"

Akasema, "Bwana, sijui uliwagharimu watu hawa nini. Lakini nina furaha sana kwamba ninaweza kuziona nyuso zao, waliolipa gharama."

50 Hivyo ndivyo tunavyojisikia. Sijui ilimgharimu nini Mungu. Ninajua alinipa kilicho bora zaidi alichokuwa nacho, Mwanawe. Lakini ninashukuru sana kuwa na macho haya ya kiroho, hata ninaweza kuutazama uso Wake na kujua kwamba alinifia. Sijui ilimgharimu nini. Hatuna njia ya kuikadiria. Bei ni kubwa mno. Nisingeweza kuwaambia jinsi ilivyo. Lakini ninashukuru. Ninashukuru, ya kwamba, ambapo wakati mmoja nilikuwa kipofu, sasa ninaweza kuona.

Ninashukuru kwamba Ndugu wa Mayo waliponiambia wakati wangu ulikuwa umekwisha, madaktari waliponiambia kwamba singeweza kuishi tena, miaka ishirini na mitano iliyopita, niko hai leo. Sijui

ilimgharimu nini Mungu, bali ninashukuru mimi ni hai.

Wakati mmoja nilikuwa mwenye dhambi, nimefungwa katika dhambi, pamoja na huzuni kuu, nikiogopa mauti. Lakini, leo, mauti ndiyo ushindi wangu. Haleluya! Ingenileta tu katika Uwepo Wake nimpendaye, kwamba niweze kuuangalia uso Wake. Yeye alibadilisha kitu hicho, kwa upasuaji, akauchukua moyo wangu na kuufanya upya. Ninajua jambo fulani lilinipata.

51 Katika gazeti moja mwaka jana, huko Minnesota, kulikuwako na mvulana mdogo aliyeichukua baiskeli yake na kwenda kanisani asubuhi moja, kwenye shule ya Jumapili. Kijana mwingine katika ujirani huo, hakushughulika na shule ya Jumapili, alimchukua rafiki yake msichana wakaenda kuteleza kwenye barafu. Naye huyo mtu alikuwa mtu mzima, ndipo akafika kwenye barafu nyembamba akaanguka. Alikuwa amemcheka huyo mvulana mdogo asubuhi hiyo alipokuwa akishuka barabarani, akamwambia rafiki yake wa kike, kasema, "Hilo ni kundi la walokole wakishuka kwenda kwenye lile kanisa." Basi alipoanguka kwenye barafu, rafiki yake wa kike alikuwa mbali naye. Alikuwa mwepesi; yeye akaepuka. Lakini alipopanda na kuweka mikono yake juu ya barafu, alipooza, na kuning'inia juu ya barafu.

Rafiki yake wa kike akajaribu kumfikia, bali alikuwa ni mzito sana, angezama barafuni. Akampigia makelele, "Rudi! Rudi! Utaanguka tu ndani, nasi sote tutazama." Akapiga makelele, akalia, wala hakuna cha kumsaidia.

52 Baada ya kitambo kidogo, huko juu ya kilima, ikaja maskini baiskeli, akipiga pedali, maskini mvulana mdogo pamoja na Biblia chini ya mkono wake. Akasikia hayo makelele, ndipo akaiendesha kasi maskini baiskeli yake. Akailaza Biblia yake chini na kukimbia kwenye barafu. Akatambaa kwa maskini tumbo lake pamoja na nguo zake nzuri, mpaka akashika mikono ya mtu huyo, na akaendelea kumvuta, mpaka akamtoa kwenye hiyo barafu. Akatoka mbio na kusimamisha gari. Wakaita gari la kuchukulia wagonjwa na kumpeleka hospitalini.

Baada ya kwenda na kulipa hilo gari la kuchukulia wagonjwa, akawalipa madaktari sindano za nimonia na vitu alivyokuwa amekunywa, akamjia maskini yule mvulana. Akasema, "Mwanangu, unaniwia nini?"

Akasema, "Hakuna."

Akasema, "Unaniwia uhai wangu." Wazia jambo hilo. Pesa hazingeweza kuulipia. Ilikuwa ni uhai wake.

53 Hivyo ndivyo tunavyopaswa kujisikia kumhusu Mungu. Sio kununua safari yetu kwa kitu fulani; bali tunawiwa na Mungu uhai wetu, kwa kuwa tulikuwa tukifa na kuzama katika shimo la dhambi. Mungu akanikumbatia kwa mikono Yake na kunivisha vazi.

Nilikuwa nikizama katika dhambi,
Mbali na pwani yenye amani,
Nimechafuka sana ndani,
Nikizama nisiinuke tena;
Lakini Bwana wa bahari
Akasikia kilio changu cha kukata tamaa,
Kutoka majini akaniinua,
Sasa niko salama.

Ninawiwa Naye maisha yangu. Unawiwa Naye maisha yako. Unawiwa Naye maisha yako, kumtumikia; si kuyatoa, kutembea huku na huko na kujigamba kuhusu kanisa lako la kimadhehebu; sio kwenda huku na huko na kuwakosoa wengine; bali kujaribu kuwatumikia na kuwaokoa wengine, na kuwaleta katika kumjua Bwana Yesu Kristo.

54 Yule mwana mpotevu. Katika kufunga, huenda nikasema hivi. Alipokwisha kufuja mali yake yote, mali ya baba yake, kwa maisha ya anasa, basi alipokuwa akirudi nyumbani… Alikuwa amelala katika zizi la nguruwe, ndipo akajirudia. Ndipo akasema, "Ni watumishi wangapi wa kuajiriwa, baba yangu anao, ambao wana chakula cha kusaza, nami hapa nafa, kwa njaa." Vipi kama angejaribu kusema, "Sijui kama nina pesa ningeweza kumlipa baba (nilizotumia katika kutangatanga) nazo?" Lakini alijua tabia ya baba yake, naye akasema, "Nitaondoka niende kwa baba yangu."

Babaye kamwe hakusema, "Ngoja kidogo, mwanangu! Je, unanirudishia pesa zangu?" La. Kamwe hakumlipisha kwa sababu ya dhambi zake. Alifurahi kwamba alikuwa anarudi. Alifurahi kwamba alikuwa amejirudia, kwa sababu alikuwa mwanawe. Alikuwa ni mtoto wake mwenyewe. Alifurahi alikuwa njiani akielekea nyumbani. Sasa, yeye hakuidhinisha dhambi yake, bali alifurahi alipojitambua na kusema, "Nimetenda dhambi mbele za Mungu wangu, na mbele ya baba yangu. Nitaondoka niende kwake."

Ndipo alipomwona, kwa mbali, alimkimbilia akambusu. Naye akasema, "Mchinjeni yule ndama aliyenona,"bila pesa. "Leteni vazi lililo bora kuliko yote," bila pesa. Leteni pete," bila pesa, "muitie kidoleni mwake. Na tule, tunywe, na tufurahi, kwa kuwa huyu mwanangu alikuwa amepotea na sasa amepatikana. Alikuwa amekufa, naye yu hai tena. Hebu na tufurahie jambo hilo."

55 Naomba niseme jambo hili marafiki, kufunga. Kitu pekee kinachoridhisha, vitu pekee vya kweli vilivyopo, vitu vizuri tu vilivyopo, haviwezi kununuliwa kwa fedha. Ni zawadi za bure za Mungu, kwa Yesu Kristo: wokovu wa nafsi; furaha. Njoni mle, mshibe.

> *Kwani kutoa fedha kwa ajili ya kitu ambacho si chakula? na mapato yenu kwa kitu ambacho hakishibishi? nisikilizeni kwa bidii, mle…kilicho chema, na kujifurahisha nafsi zenu kwa unono.*
>
> *Tegeni masikio yenu, na kunijia: sikieni, na nafsi zenu zitaishi; nami nitafanya nanyi agano la milele, naam, rehema za Daudi zilizo imara.*

56 Vitu vyote vidumuvyo, vitu vyote vyema, vitu vyote vinavyopendeza, vitu vyote vilivyo vya Milele, ni vya bure, wala havikugharimu chochote. Mwishoni mwa kuandikwa kwa Kitabu hiki, kilisema: "Atakaye, na aje anywe Maji ya chemchemi za Uzima, bure," bila pesa, bila gharama. Kwa nini kutumia fedha zako kwa kitu kisichoshibisha, na kuacha vitu halisi vinavyoshibisha, vya bure, vipotee bila kuhifadhiwa na wewe?

Hebu na tuombe.

57 Mkiwa katika utulivu na katika maombi, wapo, katika jengo hili, asubuhi ya leo, wale ambao hawajainywea Chemchemi hiyo, ambao tamaa za ulimwengu zingali katika maisha yako, na ungependa kubadilisha mahali pako pa kunywea, asubuhi ya leo, au riba ya pesa zako? Ungependa kuja na kununua kutoka kwa Mungu, (bila fedha, bila gharama), asali na maziwa, furaha ya divai? Je, waweza kuinua mkono wako, useme, "Nikumbuke, Ndugu Branham, unapoomba"? Mungu akubariki, bwana. Mungu akubariki, bwana. Mungu akubariki, dada. Kuna wengine ambao wangesema, "Nikumbuke, Ndugu Branham, unapoomba"?

58 Baadhi yenu ninyi vijana, naam, ambao mmeyaharibu maisha yenu. Zi—zi—zile saa ambazo mama alitumia katika maombi kwa ajili yako, na baba, mafundisho yote ambayo umepewa, na hata hivyo umeyaweka kando, upate kusikiliza mnong'ono wa ibilisi. Sasa unautamani muziki wa ulimwengu, mambo ya ulimwengu. Nawe unajirudia, kama yule mpotevu kwenye zizi la nguruwe. Waweza kuinua mkono wako, dada, ndugu, na kusema, "Mungu, nikumbuke. Nijalie kujirudia, asubuhi ya leo, nijalie nije nyumbani kwa Baba"? Haikugharimu hata kitu kimoja. Yeye anakutarajia. Haijalishi umefanya nini, "Dhambi zenu zijapokuwa nyekundu sana, zitakuwa nyeupe kama theluji; nyekundu kama damu, zitakuwa nyeupe kama sufu." Je, hao wako katika Uwepo wa Kiungu, ambao wangeinua mikono yao?

Wale walio wagonjwa na wahitaji, semeni, "Ni—nilianguka kwenye shimo. Shetani ame—amenitendea maovu. Amenilemaza na kunifanya mgonjwa, ama chochote kile. Ninatamani, asubuhi ya leo, mnyororo wa Mungu wa imani uingie moyoni mwangu, ambao utanitoa kwenye shimo hili, kama yule mtu kwenye lango liitwalo Zuri." Inueni mikono yenu. Mungu awabariki, kila mmoja.

59 Bwana, ninaleta Kwako, saa hii, wale wanaoinua mikono yao, kwa ajili ya msamaha wa dhambi zao. Wewe ni Mungu, na Mungu peke yako. Moja kwa moja mahali wanapoketi sasa, hapo ndipo uliponena nao. Hapo ndipo ulipowashawishi kwamba wamekosea, wakati Neno limepata mahali Pake, na Roho Mtakatifu ameanza kunena, na kusema, "Umekosea. Geuka, na uje tena kwa Mungu Baba." Nao wakainua mikono yao, kuonesha ya kwamba walitaka kutoka katika zizi hili la duniani la nguruwe, kuja nyumbani kwa Baba, ambako kuna utajiri, ambapo haitawabidi kuleta chochote. Kama vile mshairi alivyosema vyema, "Sina cha mkononi niletacho, kwa urahisi tu naushikilia msalaba Wako." Jalia waje, kwa utamu, kwa unyenyekevu, na kukiri hatia, na kuyasalimisha maisha yao. Nawe utaleta vazi lililo bora kabisa; na pete, na kuitia katika vidole vyao; na kuwalisha kwa Mana ya Mwana-Kondoo aliyechinjwa. Tujalie, Bwana.

60 Kuna wale walio wagonjwa na wanaoteseka. Wao ni wahitaji. Shetani amewatupa shimoni, hapana shaka, ukosefu wa pesa za kufanyia upasuaji. Hapana shaka, labda, wengi wao wasingeweza kufanyiwa upasuaji. Labda daktari asingeweza kuondoa chanzo chake, hata kama alikuwa na pesa nyingi sana. Lakini Wewe ni Mungu. Nami naomba ya kwamba saa ii hii, chini ya upako wa Roho Mtakatifu aliyeko sasa hivi, kwamba utamponya kila mmoja wao. Jalia waponywe, tangu kichwani mwao hata miguuni mwao, kila chembe.

Ikiwa hawana furaha; wokovu wao, hawawezi kuufurahia tena. Kama Daudi, wa kale, alivyosema, "Unirudishie furaha ya wokovu wangu." Jalia wapokee furaha na shangwe, kwa huzuni zao na uchovu wao, kwa maana Wewe ni Mwamba katika nchi ya uchovu. Wewe ni kimbilio wakati wa dhoruba. Ibilisi anapowarushia kila ugonjwa na kombora, Wewe ni kimbilio wakati wa dhoruba. Jalia iwe hivyo, leo, Mungu, kwa kuwa tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

Kwa upole na upendo Yesu anaita,
Anakuita wewe, na mimi;
Ingawa tumetenda dhambi, Yeye ana rehema na msamaha,
Msamaha kwako na kwangu.

Njoo nyumbani …

61 Sasa, ukipenda, njoo madhabahuni na upige magoti, tunaweza kuomba pamoja nawe, tukupake mafuta, chochote tuwezacho kufanya. Umekaribishwa.

…mchovu, njoo nyumbani;
Kwa bidii, kwa upole, Yesu anaita,
Anaita, Ee mwenye dhambi, njoo nyumbani!

Je! Mnampenda? Teddy, ungeweza kutupa sauti, "Nampenda, nampenda kwa sababu alinipenda kwanza." Ungeweza kupata huo?

62 Hebu na tuuimbe kwa utukufu Wake, kabla hatujabadilisha utaratibu wa ibada, kwa muda kidogo tu. Hii ni ibada. Ujumbe umetolewa. Nina furaha sana kwamba mmeupokea. Omba ya kwamba utakufanyia mema, kwa maana ulinifanyia mimi mema kuunena. Ninaomba kwamba uvuvio ule ule niliopewa, kuunena kwenu, mtaupokea kwa uvuvio ule ule uliotumiwa. Bwana na aubarikie moyoni mwenu. Vema.

Nampenda,

Sasa fumbeni tu macho yenu, tunapoimba. Tuinue mikono yetu.

Ninampenda
Kwa sababu Yeye alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Mtini pa Kalvari.

Sasa hebu na tuinamishe vichwa vyetu, tuuvumishe. [Ndugu Branham anaanza kuvumisha *Nampenda* — Mh.] Mnampenda? Yeye si halisi kwa moyo wako? Je, hakuna kitu kumhusu Yeye, ambacho ni halisi sana? Nampenda kwani alinipenda kwanza, akanitupia Kamba okozi kutoka Kalvari, akaifungia moyoni mwangu.

63 Msisahau, Ndugu Drummond atatuhubiria usiku wa leo, usiku wa ushirika. Kama unampenda Bwana, shuka uje ushiriki pamoja nasi. Bwana akipenda, nitakuwa hapa pamoja nanyi. Huyo ni mkwe wa Ndugu Tony Zabel; Ndugu Thom kutoka Afrika; mwanawe, mvulana mzuri; mzuri sana, Mkristo imara, mhubiri mzuri.

Kwa sababu Yeye alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Mtini pa Kalvari.

Huku tumeinamisha vichwa vyetu sasa, wakati piano itaendelea.

64 Bwana Yesu, tunajiandaa kuingia kwenye ibada nyingine, Bwana. Tunakushukuru kwa ajili ya Roho Mtakatifu aliyenena na mioyo yetu. Nasi tuna furaha, Bwana, ya kwamba Wewe ulitutendea jambo hili. Na jalia Neno Lako lisikurudie bure, bali na litimize lile lililokusudiwa kufanya. Jalia likae mioyoni mwetu sote, kujua ya kwamba vitu vyote halisi na vitu vya kudumu vinatoka kwa Mungu, bila pesa, bila gharama. Kwa nini basi tung'ang'anie mambo, na kulifanya jambo la kufa na kupona, kwa ajili ya mambo yatakayoangamia? Jalia tujitahidi zaidi, Bwana, kwa ajili ya mambo ambayo hayataangamia, yasiyo na gharama. . Gharama imelipwa bure, na mwaliko wa makaribisho, "Kila atakaye, na aje."

65 Bariki sehemu ifuatayo ya ibada hii. Tujalie, Bwana. Na ukutane nasi usiku wa leo. Bariki ibada ya ubatizo. Jalia kuwe na kumiminika kukubwa. Jalia watu hawa, watakaobatizwa katika Jina la Mwanao mpendwa, Bwana Yesu, jalia wajazwe na Roho Mtakatifu. Jalia watu hawa, walioinua mikono yao, watubu, asubuhi ya leo, dhambi zao, na waje, waingie ndani ya mavazi ya ubatizo, na kuingia kidimbwini, na kuuthibitishia ulimwengu kwamba wamesamehewa dhambi zao. Nao wanabatizwa, wapate kuondolewa kwenye kitabu. Tujalie, Bwana.

66 Uwe pamoja na Ndugu Drummond usiku wa leo anapotuletea ujumbe, mpya kutoka kwenye Kiti cha Enzi. Mpake mafuta kwa Roho Mtakatifu. Na uwe pamoja nasi tunaposhiriki ushirika. Mioyo yetu na iwe safi na mitakatifu, kusiwe na unajisi ndani yetu. Hebu Damu ya Yesu itusafishe na dhambi zote. Tujalie, Bwana. . Ondoa magonjwa miongoni mwetu, na utupe furaha na amani. Kupitia kwa Yesu Kristo tunaomba. Amina.

Ninapenda …

Je! Mnampenda? Sasa inueni mikono yenu Kwake.

Ninampenda
Kuwa- …

Sasa nyosha mkono na kupeana mikono na mtu fulani karibu nawe.

… kwanza …

(Russell, ninampenda. Kama nikifa leo, ninampenda.)

Na kununua …

Hiyo ni kweli, nyosha mkono na kupeana mikono.

… wokovu
Pale Kalvari …

Vema, Ndugu Neville, pamoja na neno lake. Vema.

MESSAGE hub online

www.messagehub.info

Mahubiri Na
William Marrion Branham
"... katika siku za sauti ..." Ufu. 10:7